

KUMB: PPR/19 - 12/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 4 DESEMBA 2019**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Desemba 2019**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya **Dar es Salaam**, zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Novemba 2019. Kwa mwezi Desemba 2019, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 31/lita (sawa na asilimia 1.39), Shilingi 33/lita (sawa na asilimia 1.52) na Shilingi 43/lita (sawa na asilimia 2.02), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 30.46/lita (sawa na asilimia 1.47) na Shilingi 32.63/lita (sawa na asilimia 1.60) na Shilingi 42.63/lita (sawa na asilimia 2.14), mtawalia.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga nazo zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Novemba 2019. Kwa mwezi Desemba 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimepungua kwa Shilingi 38/lita (sawa na asilimia 1.74) na Shilingi 46/lita (sawa na asilimia 2.09), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 38.04/lita (sawa na asilimia 1.84) na Shilingi 45.60/lita (sawa na asilimia 2.21), mtawalia. *Bei za Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini zitaendelea kuwa zile zilizochapishwa katika toleo la tarehe 6 Novemba 2019 kwa sababu hakuna shehena ya bidhaa hiyo iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga kwa mwezi Novemba 2019.*
- (c) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Mtwara zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Novemba 2019. Kwa mwezi Desemba 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini** (Lindi, Mtwara na Ruvuma) zimepungua kwa Shilingi 43/lita (sawa na asilimia 1.95) na Shilingi 54/lita (sawa na asilimia 2.45), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 43.34/lita (sawa na asilimia 2.06) na Shilingi 54.31/lita (sawa na asilimia 2.59), mtawalia. *Aidha, kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.*
- (d) Kwa kiasi kikubwa, punguzo la bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara linatokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (*BPS premiums*) kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.

- (e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018.****
- (h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,161	2,125	2,075
Arusha	2,215	2,198	2,123
Arumeru (Usa River)	2,215	2,198	2,123
Karatu	2,233	2,216	2,141
Longido	2,225	2,208	2,134
Monduli	2,220	2,203	2,129
Monduli-Makuyuni	2,225	2,208	2,133
Ngorongoro (Loliondo)	2,299	2,282	2,208
Pwani (Kibaha)	2,166	2,130	2,079
Bagamoyo	2,172	2,136	2,086
Chalinze Junction	2,176	2,140	2,089
Chalinze (Msata)	2,180	2,144	2,093
Kibiti	2,182	2,146	2,095

Kisarawe	2,169	2,133	2,082
Mkuranga	2,171	2,135	2,084
Rufiji	2,189	2,153	2,102
Dodoma	2,220	2,184	2,134
Bahi	2,227	2,191	2,141
Chamwino	2,215	2,179	2,129
Chemba	2,247	2,211	2,160
Konoda	2,253	2,217	2,166
Kongwa	2,217	2,181	2,131
Mpwapwa	2,221	2,185	2,135
Mtera (Makatopora)	2,239	2,203	2,152
Geita	2,327	2,291	2,240
Bukombe	2,316	2,280	2,229
Chato	2,348	2,312	2,261
Mbogwe	2,365	2,329	2,278
Nyang'hwale	2,342	2,306	2,255
Iringa	2,225	2,190	2,139
Ismani	2,231	2,195	2,144
Kilolo	2,230	2,194	2,143
Mufindi (Mafinga)	2,236	2,200	2,149
Kagera (Bukoba)	2,377	2,341	2,290
Biharamulo	2,351	2,315	2,265
Karagwe (Kayanga)	2,393	2,357	2,307
Kyerwa (Ruberwa)	2,399	2,363	2,312
Muleba	2,377	2,341	2,290
Ngara	2,365	2,329	2,278
Misenyi	2,385	2,349	2,299
Katavi (Mpanda)	2,369	2,333	2,283
Mlele (Inyonga)	2,351	2,315	2,265
Mpimbwe (Majimoto)	2,362	2,326	2,276
Tanganyika (Ikola)	2,387	2,351	2,301
Kigoma	2,393	2,357	2,306
Uvinza (Lugufu)	2,405	2,369	2,318
Buhigwe	2,382	2,346	2,295
Kakonko	2,350	2,314	2,263
Kasulu	2,379	2,343	2,292
Kibondo	2,357	2,321	2,270
Kilimanjaro (Moshi)	2,204	2,187	2,113
Hai (Bomang'ombe)	2,207	2,190	2,116
Mwanga	2,197	2,180	2,106
Rombo (Mkuu)	2,221	2,204	2,129
Same	2,190	2,173	2,099
Siha (Sanya Juu)	2,211	2,194	2,119
Lindi	2,199	2,182	2,134
Lindi-Mtama	2,204	2,187	2,152
Kilwa Masoko	2,223	2,206	2,109
Liwale	2,235	2,218	2,155
Nachingwea	2,219	2,202	2,163

Ruangwa	2,226	2,209	2,165
Manyara (Babati)	2,249	2,232	2,157
Hanang (Katesh)	2,259	2,242	2,168
Kiteto (Kibaya)	2,264	2,247	2,172
Mbulu	2,261	2,244	2,170
Simanjiro (Orkasumet)	2,281	2,264	2,189
Mara (Musoma)	2,340	2,304	2,253
Musoma Vijijini (Busekela)	2,381	2,345	2,294
Rorya (Ingirijuu)	2,349	2,313	2,262
Rorya (Shirati)	2,384	2,348	2,297
Bunda	2,331	2,295	2,244
Bunda (Kisorya)	2,341	2,305	2,254
Butiama	2,337	2,301	2,250
Serengeti (Mugumu)	2,386	2,350	2,299
Tarime	2,351	2,315	2,264
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,356	2,320	2,269
Mbeya	2,269	2,233	2,182
Chunya	2,278	2,242	2,191
Chunya (Makongolosi)	2,292	2,256	2,206
Kyela	2,284	2,248	2,198
Mbarali (Rujewa)	2,253	2,217	2,166
Rungwe (Tukuyu)	2,278	2,242	2,191
Morogoro	2,186	2,150	2,100
Mikumi	2,202	2,166	2,115
Kilombero (Ifakara)	2,224	2,188	2,138
Kilombero (Mlimba)	2,247	2,211	2,160
Kilombero (Mngeta)	2,236	2,200	2,149
Ulanga (Mahenge)	2,235	2,199	2,148
Malinyi	2,245	2,209	2,158
Kilosa	2,205	2,169	2,118
Gairo	2,205	2,169	2,118
Mvomero (Wami Sokoine)	2,197	2,161	2,110
Mvomero (Sanga Sanga)	2,186	2,150	2,100
Turiani	2,211	2,176	2,125
Mtwara	2,186	2,169	2,147
Nanyumbu (Mangaka)	2,222	2,205	2,196
Masasi	2,202	2,185	2,173
Newala	2,207	2,190	2,179
Tandahimba	2,200	2,183	2,172
Nanyamba	2,200	2,183	2,172
Mwanza	2,312	2,276	2,225
Kwimba	2,329	2,293	2,243
Magu	2,320	2,284	2,233
Misungwi	2,306	2,270	2,219
Sengerema	2,344	2,308	2,257
Ukerewe	2,371	2,335	2,284
Njombe	2,254	2,218	2,167
Njombe (Kidegembye)	2,274	2,239	2,188

Ludewa	2,292	2,256	2,205
Makambako	2,246	2,210	2,159
Makete	2,285	2,249	2,198
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,252	2,216	2,165
Rukwa (Sumbawanga)	2,334	2,298	2,248
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,334	2,298	2,248
Kalambo (Matai)	2,342	2,306	2,255
Nkasi (Namanyeke)	2,348	2,312	2,261
Ruvuma (Songea)	2,271	2,254	2,198
Mbinga	2,284	2,267	2,232
Namtumbo	2,262	2,245	2,228
Nyasa (Mbamba Bay)	2,309	2,292	2,242
Tunduru	2,237	2,220	2,257
Shinyanga	2,290	2,254	2,204
Kahama	2,304	2,268	2,217
Kishapu	2,319	2,283	2,232
Ushetu (Nyamilangano)	2,322	2,286	2,235
Simiyu (Bariadi)	2,332	2,296	2,245
Busega (Nyashimo)	2,325	2,289	2,238
Itilima (Lagangabilili)	2,335	2,299	2,248
Maswa	2,323	2,287	2,237
Meatu (Mwanhuzi)	2,330	2,294	2,244
Singida	2,252	2,216	2,165
Iramba	2,264	2,228	2,178
Manyoni	2,237	2,201	2,150
Ikungi	2,248	2,212	2,161
Mkalama (Nduguti)	2,277	2,241	2,190
Songwe (Vwawa)	2,278	2,242	2,191
Songwe (Mkwajuni)	2,285	2,249	2,198
Ileje	2,282	2,246	2,195
Momba (Chitete)	2,287	2,251	2,200
Tunduma	2,282	2,246	2,195
Tabora	2,316	2,280	2,229
Igunga	2,270	2,234	2,183
Kaliua	2,335	2,299	2,248
Ulyankulu	2,329	2,293	2,242
Nzega	2,280	2,244	2,193
Sikonge	2,327	2,291	2,241
Urambo	2,329	2,293	2,242
Uyui	2,317	2,281	2,230
Tanga	2,158	2,141	2,066
Handeni	2,178	2,161	2,087
Kilindi	2,193	2,176	2,102
Korogwe	2,170	2,153	2,079
Lushoto	2,179	2,162	2,088
Mkinga (Maramba)	2,165	2,148	2,073
Muheza	2,163	2,146	2,071
Pangani	2,164	2,147	2,073

JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,037.57	2,001.34	1,951.44

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,034.02	2,016.70	1,943.21

Bei za Jumla - MTWARA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,062.07	2,044.60	-----

JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

BANDARI YA DAR ES SALAAM

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 21.351/Tani	Punguzo la Dola 12.330/Tani	Punguzo la Dola 28.087/Tani
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (<i>BPS premiums</i>)	Ongezeko la Dola 0.824/Tani	Punguzo la Dola 4.323/Tani	Ongezeko la Dola 0.920/Tani

BANDARI YA TANGA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 18.516/Tani	Punguzo la Dola 9.231/Tani	----
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (<i>BPS premiums</i>)	Punguzo la Dola 9.300/Tani	Punguzo la Dola 9.300/Tani	----

BANDARI YA MTWARA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 21.351/Tani	Punguzo la Dola 9.267/Tani	----
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (<i>BPS premiums</i>)	Punguzo la Dola 9.300/Tani	Punguzo la Dola 9.300/Tani	----

JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

	Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mafuta yalipokelewa mwezi wa:	DSM	Novemba 2019	Novemba 2019	Novemba 2019
	Tanga	Novemba 2019	Novemba 2019	Julai 2019
	Mtwara	Novemba 2019	Novemba 2019	n/a

Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:	DSM	Oktoba 2019	Oktoba 2019	Oktoba 2019
	Tanga	Oktoba 2019	Oktoba 2019	Juni 2019
	Mtwara	Oktoba 2019	Oktoba 2019	----
Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi inayoonekana hapo juu inalinganishwa na wastani wa bei za mwezi:	DSM	Septemba 2019	Septemba 2019	Septemba 2019
	Tanga	Septemba 2019	Septemba 2019	Juni 2019
	Mtwara	Septemba 2019	----	----

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA